# WANAWAKE & DATA.

## UNAJIWEKA SALAMA MTANDAONI?



german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT


Implemented by
giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH


DIGITAL TRANSFORMATION CENTER KENYA


Co-funded by the European Union

KICTANet
The Power of Communities


KWENYE KATUNI/VIBONZO HIVI, AMANI ANAVINJARI KATIKA ULIMWENGU WA MTANDAONI PAMOJA NA KUJITOSA KATIKA 'BAHARI' YA SIASA. MARA NYINGI WANAWAKE NA WASICHANA HUJIKUTA WALENGWA WA MAMBO MABAYA MTANDAONI KAMA VILE KUNYANYASWA NA KUKANDAMIZWA KWENYE ULIMWENGU HUU UNAOZIDI KUGEUKA WA KIDIJITALI KWA HIVYO, ULINZI NA FARAGHA/SIRI YA DATA (TAARIFA ZA KIBINAFSI) YAKO NI ZANA MUHIMU YA KUKUWEZESHA KUVINJARI MTANDAONI BILA HOFU. JIFUNZE KUHUSU JINSI AMANI, KWA USAIDIZI WA RAFIKI ZAKE, ANAVYOKABILIANA NA SUALA HILI NA NAMNA NAWE PIA UNAVYOWEZA KULINDA TAARIFA ZAKO.
HALIMA
AMANI
PENDO


ZAMANI ZA KALE KATIKA NCHI YA KUFIKIRIKA YA WENYA... TULIJISHUGHULISHA SANA NA MAISHA YA MTANDAONI NA NJE YA MTANDAO...
HAMJAMBO NDUGU! KARIBUNI TENA KWENYE CHANELI YANGU! NINA TUZO BOMBA YA ZIARA ZA WATU WAWILI WATAKAOLIPIWA GHARAMA ZOTE, IWAPO KUNA YEYOTE ATAKAYEFANIKIWA KUBASHIRI KUHUSU UCHAGUZI WA MWAKA HUU NA WASHINDI!


SIKU MOJA, ALIAMUA KUWANIA URAIS, KWA HIVYO ALIZINDUA AZMA YAKE NA KAMPENI YA MTANDAONI
Amani AWANIA URAIS
AMANI
"WAWENYA WENZANGU, NINA FURAHA ISIYO NA KIFANI KUWATANGAZIA NIA YANGU YA KUWANIA URAIS! ASANTENI SANA KWA KUNIUNGA MKONO HADI SASA. IMEKUWA SAFARI YA KUFANA! PAMOJA TWAWEZA KUFIKA MBALI!"
MBASHARA: Amani atangaza nia yake mbashara


PIA KWA WAKATI HUO, WATU WOTE WA NCHI YA WENYA WALITAKIWA KUJISAJILI KWA SHUDUMA NUMBA – KADI MOJA YENYE HUDUMA ZOTE ZA UTAMBUZI WA MTU AMBAYO ILIKUSUDIWA KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA. WALIOJISAJILI, WALIFANYA HIVYO SABABU HAWAKUWA NA JAMBO LOLOTE LA KUFICHA... WALE WALIOKATAA, WALINYIMWA RUHUSA YA KUINGA MAJENGO YA SERIKALI KUPATA HUDUMA ZA UMMA HADI WATII SHARTI HILO...
BILA SHUDUMA NUMBA, HUWEZI KUINGIA
...WALA HAKUNA MTU ALIYELALAMIKIA OFISI YA KAMISHNA WA ULINZI WA DATA...


"KWA NINI WATU HAWAJISAJILI? MIYE SINA LA KUFICHA!"

RAIA WENGI WA WENYA WALIANZA KUPOKEA JUMBE ZA KAMPENI...

ILA BADO HAMNA MTU ALIYELALAMIKIA KAMISHNA WA ULINZI WA DATA

Hujambo [redacted], Asante kwa usaidizi wako. Tushirikiane kwa ajili ya kuboresha maisha yetu ya baadaye kwa kupunguza umaskini na ukosefu wa ajira. [redacted]
Jiunge nami
http://[redacted].co.ke

My [redacted] ward voter, I built boreholes and roads in [redacted] Firestation. Mimi ni surebet. [redacted]
MCA Stop*456*9*5#

Hujambo [redacted],
Nakuomba tafadhali, unipigie kura tarehe 9 Agosti nikuhudumie kama MP wa [redacted]. Asante sana. Mahitaji yako, Jukumu langu. Stop*456*9*5#

Hi [redacted],
Thanks for your support. Let's work together for the betterment of our future by alleviating poverty and unemployment. Vote [redacted] for MP [redacted] and Vote for Change!

Hujambo, Nashukuru kwa kuniunga mkono. Nakuomba kwa heshima, unipigie kura 9/8/2022 MCA [redacted] WARD.
[redacted]
No.8 on ballot
STOP *456*9*5#

Jambo, Nashukuru kwa kuniunga mkono katika azima yangu ya kuwa Nairobi Woman Rep.

Ifikapo tarehe 9/08/2022, Chagua:
[redacted]


STOP*456*9*5#



BAADHI YAO HATA WALIKUWA WAMETUMIWA DATA HII YA KIBINAFSI ILI WAITUMIE KUJARIBU KUPATA WAKE WA KUOA...
Hi! Nimekuona ukijisajili kwa Shuduma Numba. Una sura nzuri. Je, ninaweza kuja kukuchukua nyumbani kwako? Ninajua unakoishi baada ya wewe kujisajili. Ninaweza kuja na boda. Nitakununulia soda…
SHUDUMA


WAKATI HUO HUO, NAYE AMANI ALIANZA KUZIONA PICHA ZAKE ZA KIBINAFSI/FARAGHA ZIKITUMIWA KIHILA KUTENGENEZA PONOGRAFIA YA KUKARABATIWA...
HUYO SI MIMI?! NI NINI KINAFANYIKA HAPA!??
WUKO News
Prezo AMANI Aendenshwa sasa!
Video za ufichuzi za Rais AMANI
ZA KIPEKEE!
Video za ufichuzi Bofya HAPA!


WATU WALITAFUTA ALIKOISHI KISHA WAKAANZA VURUMAI NJE YA NYUMBA YAKE... ALIPOKEA SIMU NA JUMBE ZA KUMDHALIL-ISHA... NA HAKIKA WASHINDANI WAKE WA KISIASA WALIMTUSI KWELI - KIMWILI WAKATI WA MIKUTANO YA KAMPENI NA KWA MANENO MTANDAONI...
MAHASIMU WAKE WA KISIASA WALISAMBAZA NA KUZIKUKA JUMBE HIZI, WAKITUMIA TAARIFA ZA KIBINAFSI KUMWAIBISHA NA KUMTISHIA. WALIJARIBU KUTUMIA PONO HIYO YA BANDIA KUMTAPELI...
FR Yeye ni Malaya! Haifai aruhusiwe Kuwania!
MN Ni msaliti, na hata mume wake hatoki katika jamii hii!
JG Video zinazomhusu zimesambaa kote! Cheki linki hii ili ujionee... www.wukonews.com/hotgossip...
SHARTI mwaniaji huyo wa Urais AENDE! Mtu wa pono HAFAI kuwa rais!
Wewe hupata wapi pesa zako za kampeni ilhali wanawake hawaruhusiwi kumiliki ardhi! SHARTI VIONGOZI WAFISADI WAFUKUZWE!


"MIMI KWISHA... SIWEZI KUTHUBUTU KUTOKA NDANI YA NYUMBA HII YANGU... NDIPO NIKUTANE NA WATU... HATA NITAANZAJE KUFIKIRIA KUENDELEA NA KAMPENI YANGU? AU HATA KUTAFUTA KAZI BAADA YA MATUKIO HAYA YOTE??"


SAMAHANI MWENZANGU, HATA HAYO YALINIFANYIKIA NAMI PIA, SIKUGUNDUA KWAMBA NILIKUWA NA TAARIFA NYINGI ZA KIBINAFSI KWENYE MTANDAO KIASI KWAMBA HATA TULIPOKATIZA UHUSIANO WETU NA MPENZI WANGU WA ZAMANI, ALITUMIA MAELEZO YANGU YA MAWASILIANO KUENEZA UVUMI MBAYA KUNIHUSU NA KUTUMIA PICHA ZANGU KUNIHARIBIA SIFA. NILIHOFIA SANA KUINGIA MTANDAONI! KITU CHA MUHIMU NI KUPUNGUZA ZAIDI IWEZEKANAVYO TAARIFA ZINAZOKUHUSU BINAFSI MTANDAONI KAMA VILE UNAKOISHI NA UNAKOENDA, NDIPO WATU WASIWEZE KUZITUMIA DHIDI YAKO.
NDIYO DADA, NAMI NILIKUWA NA RAFIKI ALIYEANZA KUNIDUNISHA MTANDAONI KWA KUUNDA MAELEZO FEKI KUNIHUSU; KWA HIVYO NAMI PIA NILIANZA KUCHUKUA SCREENSHOTS ZA TAARIFA ZAKE NA KUANZA KUNAKILI KILA KITU CHAKE, NDIYO NAMI PIA NIWEZE KUZITUMIA DHIDI YAKE IWAPO NINGEONELEA NIFANYE HIVYO, LAKINI, HAKIKA NISINGEFURAHIA YALIYONIPATA YAMPATE MTU MWINGINE YEYOTE...


NDIYO, NILIPIGA RIPOTI KWA POLISI (OPC) PAMOJA NA DCI NILIPOANZA KUPOKEA JUMBE NYINGI ZA CHUKI. PIA NILIPIGA RIPOTI NA KUOMBA KUONDOLEWA KWENYE FB NA TWITTER. NILIKUWA NA HOFU KUWA HAKUNA KITU KINGEFANYIKA KWA KUPIGA RIPOTI HIYO LAKINI KWA HAKIKA WALINISAIDIA SANA!
YEAH, PIA JIONDOE KWA MUDA, UNAHITAJIKA KUONDOKA MTANDAONI KWA MANUFAA YA AFYA YAKO YA AKILI. UTAKAPOKUWA TAYARI TENA, TUTAKUJA KUKUSAIDIA KUREJEA MTANDAONI. HATA TUNAWEZA KUKUSAIDIA KUDHIBITI KURASA ZAKO KWA SASA KAMA UTATURUHUSU?*


ASANTENI SANA, NINAJIHISI MWENYE NGUVU MPYA NA TAYARI KUREJEA KATIKA KAMPENI ZANGU!
DCI NA ODPC WALINIFAA SANA KWA KUONDOA HIZI DHULUMA ZA MTANDAONI NA NIMEJIFUNZA MENGI KUHUSU JINSI YA KUJILINDA VYEMA ZAIDI MTANDAONI.
NINATUMAI WATU WA WENYA WAKO TAYARI...
NIKO IMARA NA BORA ZAIDI AIDHA, NI NANI ANGEJUA MAREJELEO HAYA YANGEKUWA MUHIMU!
Top chat
WTN News Kenya
Jisajili hapa kuwa
Nenda ukaendelee kufanya pono!
Nyamaza, hajawahi kufanya pono. Tunawahitaji watu wengi mfano wake kuliko wakora kama wewe!
Subscribers-only mode. Jumbe zin-azoonekana kutoka kwa watu waliojisajili kwa chaneli hii kwa dakika 5 au zaidi
LEARN MORE
Endelea Amani! Tunakuunga mkono!
Huyu ni mwendawazimu! Hawezi kuwa rais…
Amani pekee ndiye anayestahili nchi hii!
#livestream #LiveNews #WTNNews
Amani tayari kuhutubia taifa, yu tayari kurejea katika kampeni


NAO WANANCHI WA WENYA WALITIWA MOTISHA SANA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KULINDA FARAGHA YA WATU WAKE NA ULINZI WA DATA, NAO WAKAANZA KUMAKINIKIA ZAIDI ULINZI WA TAARIFA/DATA NA FARAGHA ZAO
TAMATI
8778
mtumiaji
****
8778



## FARAGHA NI NINI?

HTTPS://PRIVACYINTERNATIONAL.ORG/EXPLAINER/56/WHAT-PRIVACY

## ULINZI WA DATA NA FARAGHA YA DATA NI NINI?

FARAGHA YA DATA INAHUSU NI NANI ANAYEWEZA KUFIKIA DATA FULANI (IKIWEMO MAELEZO AU TAARIFA ZAKO ZA KIBINAFSI)

ULINZI WA FARAGHA UNAHUSU JINSI

YA KUZUIA WATU DHIDI YA KUIPATA DATA YAKO INAYOJUMUISHA TAARIFA BINAFSI ZINAZOKUHUSU.

## KWA SABABU GANI ULINZI WA DATA NA FARAGHA YA DATA NI MUHIMU?

MTU AKIACHILIA ZAIDI DATA AU TAARIFA ZAKE, ANAWEZA KUJISABABISHIA UKANDAMIZAJI, UNYANYASAJI NA AINA NYINGINEZO ZA DHULUMA NA MADHARA MTANDAONI NA NJE YA MTANDAO DHIDI YAKE AU KUNDI LA WATU. NI KIASI KINACHOSTAHILI TU CHA HABARI KUHUSU MTU NDICHO KINACHOFAA KUFIKIWA NA WATU FULANI, KWA MAKUSUDIO MAALUM NA KWA KIPINDI FULANI TU.

## HAYA YANANIHUSU MIMI AU WEWE KWA NJIA GANI?

SOTE TUNAWEZA KUCHUKUA HATUA YA KUHAKIKISHA TUNAPIGANIA NA KUTETEA ULINZI WA DATA NA FARAGHA KWA KUPUNGUZA KIASI CHA TAARIFA TUNAZOWEKA MTANDAONI, KULINDA UPATIKANAJI WA TAARIFA HIZO KWA HADHIIRA/WATU MBALIMBALI NA KUHAKIKISHA TUNADUMISHA USALAMA BORA WA MTANDAONI (IKIWEMO NYWILA YAANI NENO-SIRI AU MISIMBO THABITI, UTHIBITISHO CHANGAMANO N.K).

## JINSI YA KUIMARISHA FARAGHA NA USALAMA WAKO MTANDAONI

HTTPS://HELPDESKGEEK.COM/HOW-TO/HOW-TO-IMPROVE-YOUR-ONLINE-PRIVACY-AND-SECURITY/

## HAKI ZA WANAWAKE MTANDAONI

VIDOKEZO KUHUSU MAISHA SALAMA KIDIJITALI HTTPS://EDRI.ORG/OUR-WORK/WOMENS-RIGHTS-ONLINE-TIPS-FOR-A-SAFER-DIGITAL-LIFE/

ULINZI WA DATA NA FARAGHA. MTAZAMO WA KIJINSIA HTTPS://WWW.KICTANET.OR.KE/MDOCS-POSTS/DATA-PROTECTION-AND-PRIVACY-A-GENDER-PERSPECTIVE/

## NI WAPI NINAPOWEZA KUPATA MAELEZO ZAIDI KUHUSU ULINZI WA DATA NA FARAGHA?

ORODHA YA MAREJELEO:

WWW.KICTANET.OR.KE
WWW.APC.ORG
WWW.ARTICLE19.ORG
WWW.ACCESSNOW.ORG
WWW.UNESCO.ORG
WWW.ATINGI.ORG



# WANAWAKE & DATA.

# UNAJIWEKA SALAMA MTANDAONI?


IMEANDIKWA NA RIVA JALIPA

MICHORO YA NZILANI SIMU

VIONGOZI WA MRADI LIZ OREMBO, ANGELA MINAYO & GRACE GITHAIGA



german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by
giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

DIGITAL TRANSFORMATION CENTER KENYA

Co-funded by the European Union

KICTANet
The Power of Communities